**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA**

**VIJIJINI SHULE YA SEKONDARI KILI**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KILI MWAKA 2024

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA VIJIJINI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 0787 295714/0769 590 997**

**Makamu Mkuu wa Shule:0782785288**

**Shule ya Sekondari Kili**

**S.L.P.4**

**Bukene**

**Tarehe:17.04.2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………**
**…………………………………**
**S.L.P ……………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KILI HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA DC MKOA WA TABORA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya HGK,HGL,HGLi na HGFa.

Shule ya Sekondari KILI ipo umbali wa Kilometa 40 kutoka Nzega mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Nzega mjini Nauli ni Shilingi 5000 kwa basi na kutoka kituo cha Bukene hadi shuleni nauli ni shilingi 2000 kwa pikipiki.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01.07.2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01.07.2024.

**Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

(a) Shati mbili nyeupe mikono mirefu (zitakaguliwa).
(b) Viatu pea mbili vyeusi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba.
(c) Soksi nyeupe ndefu pea mbili.
(d) Sketi mbili rangi damu ya mzee (mshono rinda box ndefu hadi kisiginoni).



(e) Sweta rangi damu ya mzee mbili mshono alama ya V shingoni.
(f) Tai rangi damu ya mzee mbili.
(g) Hijabu rangi nyeupe mbili( Shungi refu na isiwe mtandio)
(h) Nguo za kushindia sketi rangi nyeusi (mshono rinda box ndefu hadi kisiginoni).
(i) Tisheti rangi ya kijivu yenye kola ya kijivu. (Aje amevaa pamoja na sketi nyeusi).
(j) Tisheti rangi ya damu ya mzee yenye kola nyeupe.

**Nguo za Michezo:**

A. Track suit rangi ya blue bahari pea 1,
B. raba jozi moja ya kufunga na kamba.

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 7.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;
iv. Calculator;
v. Godoro la sponji futi 2½ kwa 6.
vi. Mashuka Jozi 2 rangi bluubahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 futi 3½ kwa sita *;*
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula: Sahani ya bati 1, Bakuli ya bati 1, Kijiko na umma, Kikombe cha bati 1,Ndoo za plastiki 2 zenye mifuniko.
ix. Kwanja 1,panga 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na wa nje.

**Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule kwa (Msiba au Ugonjwa**).

- **Mwanafunzi kamwe haruhusiwi kuja na nguo za kawaida(za nyumbani).**

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KILI.**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ……………………………………………

**Jina la Mkuu wa Shule: ESTON KATIRIGE**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**……………………………………

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KILI
S. L. P. 4
BUKENE

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0787 295714/0769 590 997**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0782785288**
- **Mwandamizi Taaluma :0762623897**
- **Mwandamizi Malezi :0629160056**

**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA**
**SHULE YA SEKONDARI KILI**

---

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a government Medical Officer and returned to the Head master Kili Secondary School)

NAME…………………………………………………………………………………………………

(Please examine the student named above and comment on his/her hearth recording to the following items. Kindly put a tick in out of either TES or NO whichever is applicable)

1. Does the student have problem in connection with
   A. Sight? …………………………………………………… 1. NO ………..……………….
      IF YES State……………………………………………… 2. YES ……………………..…
   B. Hearing?........................................................................ 1. NO………………………..
      IF YES State……………………………….…………… 2. YES ………………………
   C. TB……………………..………………………………….. 1. NO ………………………..
      IF YES State…………………………………...……. 2. YES ………………………
   D. Blood pressure ……………………………………..…….. 1. NO ……..…………………
      IF YES State…………………………………………..… 2. YES ………..……………
   E. Any other health problems………………………………... 1. NO …………..…………
      IF YES State…………………………………………..… 2. YES …………….………
   F. Syphilis and other veneral diseases……………………………. 1. NO ……………………
      IF YES State……………………………...……………. 2. YES ……………………
   L. No please State………………………………………………………………………..…

Name and signature…………………………………………Designation............………………

…………………………… Date………………………….. Official stamp